


# Je, watoto wagonjwa wanapaswa kukaa nyumbani kutoka kwenye huduma ya malezi kwa watoto au shule ya msingi wakati gani?



## 1. Je, mtoto wako amekuwa na homa, kikohozi, maumivu kwenye koo, au pua yenye msongamano saa 24 zilizopita?




Lazima mtoto wako akae nyumbani au kutoka kwenye huduma ya malezi kwa watoto au shule ya msingi. Ikiwa hali yam toto itazidi kuwa mbaya na/au una wasiwasi, wasiliana na daktari wa mtoto wako au huduma ya matibabu ya baada ya saa za kazi

## 2. Je, mtoto wako bado ni mgonjwa baada ya saa 48?



NDIYO

Wasiliana na daktari au huduma za matibabu za baada ya saa za kazi ikiwa mtoto wako hajapona. Daktari ataamua ikiwa mtoto wako anapaswa kupimwa COVID-19.



HAPANA


Mtoto wako anaweza kuenda kwenye huduma ya malezi kwa watoto au shuleni anapoonekana kuwa na hali njema na hana homa. Mtoto anaweza kuenda kwenye huduma ya malezi kwa watoto au shule ya msingi hata ikiwa bado ana dalili kidogo kama vile kamasi, amepwelewa sauti kidogo au ana kikohozi kidogo. Si lazima mtoto apimwe COVID-19.

## 3. Je, mtoto wako anapaswa kupimwa COVID-19?



NDIYO

Lazima mtoto wako akae nyumbani hadi upokee matokeo ya vipimo.



HAPANA

Mtoto wako anaweza kuenda kwenye huduma ya malezi kwa watoto au shuleni anapoonekana kuwa na hali njema na hana homa. Mtoto anaweza kuenda kwenye huduma ya malezi kwa watoto au shule ya msingi hata ikiwa bado ana dalili kidogo kama vile kamasi, amepwelewa sauti kidogo au ana kikohozi kidogo.

## 4. Je, mtoto wako ana COVID-19?



NDIYO

Lazima mtoto wako akae nyumbani. Manispaa yatakuambia sheria ambazo laziima wewe na familia mfuatae mtoto akiwa mgonjwa.



HAPANA

Mtoto wako anaweza kuenda kwenye huduma ya malezi kwa watoto au shuleni anapoonekana kuwa na hali njema na hana homa. Mtoto anaweza kuenda kwenye huduma ya malezi kwa watoto au shule ya msingi hata ikiwa bado ana dalili kidogo kama vile kamasi, amepwelewa sauti kidogo au ana kikohozi kidogo.

## Wasiliana na daktari wako au huduma za matibabu za baada ya saa za kazi ikiwa mtoto ana mafua na:

- Mtoto hataki kucheza au kushughulika.
- Mtoto ana homa, maumivu ya misuli, hana hamu ya kula, uchovu, kichefuchefu au kizunguzungu.
- Matatizo ya kupumua na/au kupumua haraka kuliko kawaida anapopumzika.
- Kumbuka kuwa watoto wadogo hawawezi kueleza jinsi wanavyohisi, huenda wakawa wanalialia, kutotaka kutenganishwa au kuwashwa.